TANGAZO LA SERIKALI NA. 97 la tarehe 9/2/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1)*

SHERIA NDOGO YA (USAFI WA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU YA MWAKA 2024.

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka au kupima afya;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa dawa;

"choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya

kudumu;

"chukizo" au kero" maana yake ni kitu chochote kilicho katika hali yoyote ambacho kinatumika, kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;

(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa;

(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Magu;

"jengo la biashara" maana yake jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya biashara iliyokusudiwa;

"kaya" maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto wanaoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye eneo la Halmashauri;

"kizimba cha taka" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu;

"mabwawa ya maji taka" maana yake ni mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani na viwanda;

Sura ya 191

"maji taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Sura ya 191

"taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

**4**. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi anayeishi au anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara kuhakikisha kwamba-

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;
(b) taka zote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;
(c) anachimba shimo la kutupa taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi tatu na upana usiopungua futi mbili;
(d) anajenga choo imara cha kudumu kwa matofali na kuezeka kwa bati, tembe, majani au vigae chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuna chombo cha maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono;
(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi; na
(f) maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Uhifadhi wa maji taka

**5**. Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhia maji taka;
(b) kunyonya maji taka kila wakati karo linapojaa; na
(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote ambayo haijatengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji taka.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

**6**. Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa kutimiza masharti na kanuni za afya.

Upimaji wa afya

**7**. Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, nyumba ya kulala wageni, bucha, muoka mikate au mtu anayeshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa kuhakikisha kwamba anapima afya yake kila baada ya miezi sita.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

**8**.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote ndani ya Halmashauri kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kushauri au kuelekeza watu au mtu kutokuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuzuia shughuli mbalimbali wakati wa mlipuko wa magonjwa ikiwa ni pamoja na kukamata vyombo au vifaa vingine vinavyotumika na ambavyo vinaweza kuleta madhara kwa wakazi wa Halmashari.

(4) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kufunga au kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Vifaa vya kuhifadhia taka ngumu

**9**.-(1) Kila mmliki wa jengo la makazi, mpangaji wa jengo la makazi au mtu yeyote anayefanya biashara katika eneo lolote ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhia taka chenye mfuniko na atawajibika kukusanya taka hizo kwenye vizimba vya kuzolea taka katika maeneo yaliyoainishwa.

(2) Kila mmiliki wa jengo au mpangaji wa nyumba iliyo katika ukanda wa kijani, katika maeneo ambayo hayajapimwa atalazimika kuwa na shimo kubwa la kukusanya taka ngumu katika eneo lake.

Ada ya uzoaji taka

**10**. Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika vizimba vya taka vilivyoainishwa katika kila kata, na wazalishaji taka watalipia ada au ushuru wa ukusanyaji wa taka kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji wa taka ngumu

**11**.-(1) Hairuhusiwi kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa au chombo chochote cha taka ngumu au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye pipa au chombo cha taka zitabaki kuwa mali ya mkazi au mmliki wa eneo lile mpaka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye kizimba cha taka au zitakapokuwa zimetolewa na Wakala kutoka katika eneo lake.

Eneo la kutupa taka

**12**. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupa taka;

(b) kuweka vyombo maalumu vya kutunza taka katika maeneo ya Halmashauri; na

(c) kutoa huduma ya uzoaji takataka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

Kibali cha kusafirisha taka za plastiki

**13**.-(1) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha taka za plastiki zinazosafirishwa kwa ajili ya urejelezaji .

(2) Magari binafsi yatakayokuwa yanasafirisha taka za palstiki kutoka maeneo ya uzalishaji yatapaswa kusajiliwa na kupewa kibali kwa kulipa ada ya shilingi elfu ishirini tu kwa mwaka.

(4) Mtu yeyote atakayekusanya taka za plastiki kutoka kwa wanaozichambua katika eneo la uzalishaji au vituo vya kukusanyia atatakiwa kupata kibali na kulipa ada ya shilingi elfu ishirini kwa mwaka.

(5) Kibali cha kusafirisha taka za plastiki kitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

Wajibu wa mmiliki wa duka la kuuza nyama

**14**. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuza nyama kuhakikisha kwamba-

(a) ana jengo la kudumu lililosakafiwa na kuwekwa marumaru nyeupe kwenye sakafu na kuta kwa urefu wa futi sita kutoka usawa wa sakafu;
(b) jengo lina maji safi, gogo na misumeno ya kukatia nyama;
(c) kuna pipa la kuhifadhia taka;
(d) mhudumu ana koti jeupe pamoja na viatu vyeupe aina ya buti; na
(e) mhudumu anapima afya kila baada ya miezi sita.

Siku ya usafi

**15**.-(1) Kila jumamosi ya wiki ya pili na jumamosi ya wiki ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalamu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya Halmashauri.

(2) Itakuwa ni wajibu kwa kila mkazi katika kijiji na kitongoji kushiriki katika usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika maeneo yao na maeneo ya umma.

(3) Kila mtu atahakikisha kuwa eneo lake la makazi, eneo linalomzunguka, eneo analofanyia biashara, eneo la wazi lililokaribu naye kwa umbali wa mita kumi na eneo la mazingira ya ofisi ni safi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Vikundi vya usafi

**16**. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika vijiji na vitongoji baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

**17**. Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika na kuchafua mazingira.

Mabaki ya ujenzi

**18**. Mtu yeyote hataruhusiwa kubomoa au

kusababisha kubomoka kwa jengo au sehemu ya jengo bila kutoa taarifa ya maandishi kwa Halmashauri siku saba kabla ya kubomoa jengo.

Udhibiti utupaji wa taka

**19**.-(1) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma hawataruhusiwa-

(a) kutupa taka nje ya vyombo wanavyotumia na taka zote zitawekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo husika; au
(b) kutupa taka ovyo katika maeneo ya makazi, biashara, mifereji ya maji ya mvua, hifadhi ya barabara au mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

(2) Mtu yeyote au mkazi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalumu vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalumu yaliyotengwa.

Uhifadhi wamaji taka

**19**.-(1) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufungulia na kutiririsha maji taka au kinyesi kutoka chooni au sehemu yoyote wakati wa mvua au wakati wowote kwenye mifereji ya maji ya mvua, mabonde au maji yanayotembea au sehemu nyingine yoyote isiyoruhusiwa.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

**20**. Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba-

(a) nyumba yake ina choo boira kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo;
(b) anaweka sehemu maalumu ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni ya kimiminika; na
(c) choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini kutoka chanzo chochote cha maji.

Vyoo vya

**21**.-(1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma

umma

au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa kuwa vya kudumu na-

(a) matundu yasiyopungua mawili kwa wanawake na mawili kwa wanaume;
(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama;
(c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba;
(d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake;
(e) kuwepo na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na
(f) kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

**22**. Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu na atatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

**23**. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo bora vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsi zote.

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

**24**.-(1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

(2) Ilani ya kujenga au kurekebisha choo itakuwa katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Nne.

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa

**25**. Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote

ya mlipuko

kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wakati wa zuio

**26**.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka, Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka, Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Ilani ya kuondoa kero

**27**.-(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Ilani ya kuondoa kero itakuwa katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Uteuzi wa wakala

**28**.-(1) Halmashauri inaweza kumteua wakala kwa ajili ya kutoa huduma ya usafishaji na ukusanyaji wa taka kwa niaba yake.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa-

(a) ameingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kutoa huduma ya usafi wa mazingira; na

(b) anakusanya na kutupa taka hizo kwenye dampo kuu la Halmashauri.

Makosa

**29**. Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa endapo-

(a) atatupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo;

(b) atamzuia au kujaribu kumzuia au kumshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;

(c) atamwaga taka barabarani, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(f) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(g) atapika vyakula pembezoni mwa barabara au nje ya majengo mengine;

(h) atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi na kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(i) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(j) atavuta sigara hadharani au mahali pa jumuiya au kwenye vyombo vya usafiri;

(k) atatema mate hovyo au kutema mate barabarani au mahali pa jumuiya;

(l) ataacha nyumba anayoishi au kumiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo;

(m) ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;
(n) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;
(o) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi;
(p) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni au upenuni; au
(q) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri;

Adhabu

**30**. Mtu atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

**31**. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10)*

GHARAMA ZA UKUSANYAJI TAKA KATIKA MAJENGO YA BIASHARA NA MAKAZI

| Namba | Aina ya Biashara | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Aina nyingine ya biashara/huduma | 10,000 kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Baa | 4,000 kwa mwezi |
| 3 | Benki | 10,000 kwa mwezi |
| 4 | Dahalia (Hostel) | 10,000 kwa mwezi |
| 5 | Dobi mdogo | 1000 kwa mwezi |
| 6 | Dobi Mkubwa | 2,000 kwa mwezi |
| 7 | Duka la simu, kampuni ya simu kwa mnara | 10,000 kwa mwezi |
| 8 | Duka dogo la chakula (mini Supermarket) | 3,000 kwa mwezi |
| 9 | Duka kubwa la chakula (Supermarket) | 5,000 kwa mwezi |
| 10 | Duka la dawa (rejareja) | 5,000 kwa mwezi |
| 11 | Duka la dawa (Jumla ) | 10,000 kwa mwezi |
| 12 | Duka la Jumla | 5,000 kwa mwezi |
| 13 | Duka la kuuza nyama na samaki | 5,000 kwa mwezi |
| 14 | Duka la Nguo | 3,000 kwa mwezi |
| 15 | Duka la rejareja bidhaa mchanganyiko | 5,000 kwa mwezi |
| 16 | duka la vifaa chakavu | 5,000 kwa mwezi |
| 17 | Duka la vinywaji na chakula (grocery) | 2,000 kwa mwezi |
| 18 | Fundi chuma | 2,000 kwa mwezi |
| 19 | Fundi Seremala | 2,000 kwa mwezi |
| 20 | fundi viatu | 1,000 kwa mwezi |
| 21 | Fundi wa kushona kwa kila cherehani | 1,000 kwa mwezi |
| 22 | Fundi wa vifaa vya umeme | 3,000 kwa mwezi |
| 23 | Genge kwa meza moja | 1,000 kwa mwezi |
| 24 | Gereji pikipiki | 5,000 kwa mwezi |
| 25 | Gereji ya magari | 10,000 kwa mwezi |
| 26 | Ghala | 10,000 kwa mwezi |
| 27 | Karakana | 10,000 kwa mwezi |
| 28 | Kituo cha Afya (taka zisizo hatari) | 10,000 kwa mwezi |
| 29 | kituo cha baiskeli | 3,000 kwa mwezi |
| 30 | kituo cha boda boda | 10,000 kwa mwezi |
| 31 | Kituo cha kuuza mafuta | 50,000 kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 32 | Kituo cha kuuzia gesi | 5,000 kwa mwezi |
| 33 | Kituo cha michezo | 5,000 kwa mwezi |
| 34 | kiwanda cha kuuza mbao | 10,000 kwa mwezi |
| 35 | Kiwanda kidogo | 10,000 kwa mwezi |
| 36 | Kiwanda kidogo kwa trip zisizozidi 4 kwa mwezi | 10,000 kwa mwezi |
| 37 | Kiwanda kikubwa | 100,000 kwa mwezi |
| 38 | Klabu ya pombe ya asili | 5,000 kwa mwezi |
| 39 | Klabu ya usiku | 8,000 kwa mwezi |
| 40 | Kumbi za starehe | 10,000 kwa mwezi |
| 41 | Lori la Mizigo kushusha (mzigo eneo rasmi) | 5,000 kwa tripu moja |
| 42 | Maabara ya Vipimo | 10,000 kwa mwezi |
| 43 | Madawa ya asili | 5,000 kwa mwezi |
| 44 | Makazi (kaya) kijijini | 1,000 kwa mwezi |
| 45 | Makazi (kaya) Mjini | 2,000 kwa mwezi |
| 46 | Mama lishe/baba lishe | 1,000 kwa mwezi |
| 47 | Mashamba makubwa ya maua, kahawa, kahawa na mazao mengine | 100,000 kwa mwezi |
| 48 | Mgahawa Mkubwa | 5,000 kwa mwezi |
| 49 | msikiti/kanisa bila kuwa na shughuli za biashara | 10,000 kwa mwezi |
| 50 | Nyumba ya Kulala wageni | 10,000 kwa mwezi |
| 51 | Nyumba kwa ajili ya watumishi (Watumishi Housing) | 100,000 kwa mwezi |
| 52 | Ofisi za ulinzi | 5000 kwa mwezi |
| 53 | Saluni | 3,000 kwa mwezi |
| 54 | sehemu za kutengeza chai/uji na vitafunwa | 1,000 kwa mwezi |
| 55 | Shughuli za vioo | 10,000 kwa mwezi |
| 56 | Shule ya Msingi ya Bweni binafsi | 10,000 kwa mwezi |
| 57 | Shule ya Msingi ya kutwa binafsi | 10,000 kwa mwezi |
| 58 | Shule ya sekondari kutwa binafsi | 10,000 kwa mwezi |
| 59 | shule ya sekondari ya bweni | 10,000 kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 60 | Stoo | 10,000 kwa mwezi |
| 61 | Stoo za Mkaa | 10,000 kwa mwezi |
| 62 | Taasisi/Idara | 10,000 kwa mwezi |
| 63 | Uwanja wa michezo | 20,000 kwa mwezi |
| 64 | Vibanda kuweka na kutoa fedha | 1,000 kwa mwezi |
| 65 | Vifaa vya ujenzi | 4,000 kwa mwezi |
| 66 | vifaa vya umeme, simu, | 4,000 kwa mwezi |
| 67 | Vipuri na Vifaa | 2,000 kwa mwezi |
| 68 | Vitabu shajala | 2,000 kwa mwezi |
| 69 | Vituo vya kuoshea magari | 10,000 kwa mwezi |
| 70 | Kuuza miwa (kwa kituo) | 5,000 Kwa mwezi |

____________

**JEDWALI LA PILI**

____________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 27(2))*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**
**ILANI YA KUONDOA KERO**

**SEHEMU 'A'**

Ndugu……………………………………………… wa Mtaa/Kijiji………………………Kata ya……………….unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……......mwezi…………mwaka………… katika nyumba yako ya Biashara/Kuishi/Kutolea Huduma* iliyopo eneo la……………………………….kumekutwa na adha zifuatazo:

1. ………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………
5. ………………………………………………………………………

**SEHEMU 'B'**

Kwa ilani hii unaamriwa kufanya yafuatayo:

1. …………………………………………………………………………
2. …………………………………………………………………………
3. …………………………………………………………………………
4. …………………………………………………………………………
5. …………………………………………………………………………

**SEHEMU 'C'**

*Tanagazo La Serikali Na. 97 (Linaendelea)*

Unapewa muda wa siku ……… tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza yote yaliyoelezwa katika Sehemu 'B' ya ilani hii. Kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

**IMEPOKELEWA NA:**
Jina……………………………. ……
Saini…………………………… ……
Wadhifa………………………………
Tarehe…………………………. ……

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**
Kimetolewa na:

Jina la Afisa Mwidhiniwa…………………………………..Saini………

Wadhifa:…………………………………………………………..

Tarehe:…………………

Muhuri:……………………………………………

*futa lisilohusika

**JEDWALI LA TATU**

**KIBALI CHA KUSAFIRISHA TAKA ZA PLASTIKI**
*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13(4))*

Namba ya Kibali…………………… ……………………………………..
Jina…………………………………………………………………………
Anwani: ……………………………………………………………………………………
Umeruhusiwa kusafirisha taka ngumu kutoka: ……………………Kata/Wilaya)
Kwenda ……………………………… Kata/Wilaya.
Aina ya Gari na Namba ya usajiri wa Gari lililopewa kibali cha Kusafirisha …………………………………… Leseni hii itatumika kuanzia………20………………….Hadi……………20…………………………

Leseni hii imetolewa kwa kuzingatia masharti yafuatayo……………………………………………………………………………………………
………………………………

…………………………………………………………………………………………………………
………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**
Kimetolewa na:
Jina la Afisa Mwidhiniwa…………………………………..Saini………
Wadhifa:………………………………………………………………..
Tarehe:…………………
Muhuri:……………………………………………
*futa lisilohusika

**JEDWALI LA NNE**

**ILANI YA KUJENGA AU KUREKEBISHA CHOO**
*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 24(2))*

**SEHEMU 'A'**
Ndugu…………………………………………wa Mtaa/Kijiji……………Kata ya……………………………………………..Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe………..Mwezi…………Mwaka……………… Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea huduma* namba..…………………iliyopo eneo la……………………..………… Katika kitongoji/Mtaa*……………Kijiji cha…………………Kata ya………………… Imekuwa haina choo/choo kimejaa/kimeharibika * hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo:-
(1)………………………………………………………………………………
(2)………………………………………………………………………………
(3)………………………………………………………………………………
(4)………………………………………………………………………………

**SEHEMU 'B'**
Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelekezwa katika sehemu 'A' ya Ilani hii.

**SEHEMU 'C'**
Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe…………… endapo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itachukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

**IMEPOKELEWA NA:**
Jina……………………………. ……
Saini…………………………… ……
Wadhifa………………………………
Tarehe…………………………. ……

*Tanagazo La Serikali Na. 97 (Linaendelea)*

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**
Kimetolewa na:
Jina la Afisa Mwidhiniwa…………………………………..Saini………
Wadhifa:……………………………………………………………..
Tarehe:…………………
Muhuri:……………………………………………
*futa lisilohusika

---

**JEDWALI LA TANO**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 31)*

**FOMU YA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi;…………………………………………………….. nakiri **KWA HIARI YANGU MWENYEWE** mbele ya;…………………………………ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Magu, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;….…. Mwaka;…….… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya……….. ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:**

Leo tarehe:…....... ya Mwezi:………… Mwaka:…………..
Jina:……………………………..…………………….
Saini:………………………...……………………………
**MBELE YANGU:**
Jina:…………………………..………..……………………
Wadhifa:……………………………………………..…….
Saini:………………………………………………………
Tarehe:……………………………………………………

Nembo na mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika Tarehe 27 Mwezi machi Mwaka 2022

FIDELIKA GABRIEL MYOVELLA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Magu*

MPNDALUME S. MPANDALUME
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Magu*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Februari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB),
*Waziri Wa Nchi - Ofisi Raisi,*
*(Tawala Za Mikoa Na Serikali Za Mitaa)*